JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI

WAKALA YA BARABARA TANZANIA

Tarehe 11/11/2026

TAARIFA KWA UMMA

WITO WA KUZINGATIA USALAMA BARABARANI WAKATI WA KUANZA KWA KAZI ZA UJENZI WA BARABARA YA CHAMWINO–DODOMA

Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) inatoa wito kwa watumiaji wote wa barabara na wananchi kwa ujumla kuzingatia tahadhari za usalama kufuatia kuanza kwa kazi za ujenzi wa barabara ya Chamwino–Dodoma yenye urefu wa kilomita 32.

Kazi za ujenzi zimeanza katika eneo la Ihumwa, ambapo kutakuwa na mabadiliko ya muda ya mpangilio wa matumizi ya barabara na uelekezaji wa magari katika baadhi ya maeneo ili kuruhusu shughuli za ujenzi kufanyika kwa usalama.

Hivyo, watumiaji wa barabara wanatakiwa kuzingatia alama na michoro ya muda, kufuata maelekezo ya waongoza magari na askari wa usalama barabarani, kutumia njia zilizoelekezwa, kupunguza mwendo na kuepuka kuingia katika maeneo ya kazi za ujenzi.

TANROADS inasisitiza umuhimu wa ushirikiano kwa watumiaji wa barabara katika kuzuia ajali na kulinda usalama wa wananchi pamoja na wafanyakazi wanaoshiriki katika kazi za ujenzi.

Aidha, Wakala inaomba wananchi kuwa na uvumilivu na kushirikiana na timu za mradi katika kipindi chote cha ujenzi, huku ikiomba radhi kwa usumbufu wowote wa muda utakaoweza kujitokeza.

“USUMBUFU WA MUDA, MAENDELEO YA KUDUMU”

Imetolewa na:

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano,
Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS).

Njedengwa Investment Area, Block F, Plot No. 8, 8 Uchaguzi Road, P.O Box 2433, Dodoma,
Telephone: +255262310080-5, Fax: +255262310087/8/9/0,
Email: tanroadshq@tanroads.go.tz, website: www.tanroads.go.tz